## Maswali

1. Nani alikuwa mfalme wa Babeli?
2. Mfalme Dario alimfanya nani mtawala wa maana?
3. Mbona mawaziri walitaka Danieli apatikane kwa makosa?
4. Mawaziri walipata Danieli kuwa amefanya makosa yoyote?
5. Mawaziri walikuwa na mpango gani?
6. Danieli alifanya nini aliposikia juu ya sheria mpya?
7. Mbona Mfalme Dario hakuweza kuokoa Danieli kutoka kwa simba?
8. Nini ilifanyika Danieli alipotupwa ndani ya tundu la simba?
9. Mbona Mfalme Dario alifurahi ilipofika asubuhi?
10. Nini ilifanyika kwa mawaziri waovu?

## Majibu

1. Dario alikuwa mfalme wa Babeli.
2. Mfalme Dario alimfanya Danieli mtawala wa maana.
3. Mawaziri walikuwa na wivu kwa sababu alifanywa mtawala juu yao.
4. Hapana. Mawaziri hawakupata Danieli na makosa yoyote.
5. Waliuliza mfalme aweke amri kwamba mtu yeyote akiomba dua kwa mtu mwingine asipokuwa mfalme, atatupwa kwa tundu la simba.
6. Danieli aliendelea kuomba Mungu mara 3 kwa siku.
7. Sheria haingebadilishwa.
8. Mungu alituma malaika wakashika midomo ya simba.
9. Mfalme Dario alifurahi kwa sababu Mungu alikuwa amemwokoa Danieli kutoka kwa simba.
10. Mawaziri waovu walitupwa ndani ya tundu la simba na wakafa.

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 1 Mwaka wa 3**

# 33 Danieli katika tundu la simba

## Marejeo

Danieli mlango wa 6

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu anaweza kuokoa wanaompenda na kumwamini.

## Maneno maalum

33.1 Daniel + Mfalme Dario + mtawala wa maana + mawaziri + wivu + Danieli + shida

33.2 Mpango + Danieli anaomba + sheria mpya + omba dua kwa mfalme peke + adhabu + tundu la simba

33.3 Danieli + jasiri + omba Mungu + mawaziri walichunguza

33.4 Mfalme Dario + sikitika + sheria haibadiliki + Danieli + tundu la simba + mfalme hakulala + Mungu aliokoa Danieli?

33.5 Mfalme Dario + Mungu amekuokoa? + funga midomo ya simba + Danieli aliokoka + mawaziri waovu + tubwa kwa simba

**33.1** Danieli aliishi Babeli, lakini Mfalme Nabukadreza alikuwa amekufa na kulikuwa na mfalme mwingine aliyeitwa Dario. Mfalme Dario alitawala nchi kubwa kwa hivyo alikuwa na mawaziri 120 wakumsaidia. Juu ya hawa mawaziri, kulikuwa na watatu waliokuwa wa maana zaidi. Danieli alikuwa wa maana zaidi kwa hawa watu watatu.

Mfalme Dario alijua Danieli alikuwa mtu mzuri tena ana hekima. Dario aliamua kumfanya Danieli kutawala ufalme wake wote. Lakini mawaziri waliposikia hayo, waliona wivu sana. Hawakutaka Danieli awe wa maana kuliko wao. Walijaribu kutafuta makosa kwa Danieli ili waambie mfalme na ipatikane kwamba Danieli ni mbaya na awe kwa shida.

Lakini Danieli alikuwa mtawala mzuri sana tena mtu mwaminifu. Mawaziri waliendelea kuchunguza Danieli kwa muda mrefu lakini hawakupata kitu cho chote alichofanya kibaya.

**33.2** Halafu mmoja wao akawa na mpango ulioonekana ni mzuri sana. Walijua kwamba Danieli kila mara alipiga magoti karibu na dirisha lake akiomba Mungu mara tatu kwa siku. Walizungumuzia huo mpango na wakaenda kuona Mfalme Dario.

Waliambia Dario, "Mawaziri wote wamefikiria kwamba ingekuwa vyema kama sheria ingetengenezwa ya kusema kwamba kwa mwezi moja kila mtu akuzujudie wewe Mfalme Dario kama mungu wao. Mtu yeyote atakayeomba mungu mwingine kando ya wewe, atatubwa kwenye tundu la simba." Mfalme akaona kwamba hii ni sheria nzuri. Aliona hii itamfanya awe na mamlaka makubwa kwa ufalme wake. Kwa hivyo alifanya hiyo sheria na kila mtu akaisikia.

**33.3** Halafu mawaziri walianza kumchunguza Danieli. Walichunguza ili wamwone kama atavunja sheria mpya kwa kuendelea kuomba Mungu kila siku. Danieli alijua kwamba hataacha kuomba Mungu wake. Lazima ataabudu Mungu hata kama atatubwa kwenye tundu la simba.

Danieli alikuwa mjasiri sana kwa sababu alijua Mungu atamsaidia. Mara tatu kwa siku alipiga magoti kwa chumba chake na kuomba Mungu kama kawaida. Mawaziri walimwonea kwa dirisha lililokuwa wazi na wakaenda kuambia Mfalme Dario.

**33.4** Mfalme Dario aliposikia hayo alisikitikia Danieli sana kwa sababu aliweka sahihi kwa hiyo sheria. Alijua kwamba ulikuwa mpango wa hao mawaziri wenye wivu ili wamshike Danieli kwenye makosa. Mfalme Dario alijaribu kuokoa Danieli asitupwe kwa simba. Lakini sheria ilikuwa imetengenezwa na haingebadilishwa. Jioni hiyo Dario alimwita Danieli. Alimwambia, "Hebu Mungu wako, unayemtumikia, akuokoe kutoka kwa simba." Halafu Danieli alitupwa kwenye tundu la simba.

Mfalme hakuweza kulala usiku huo. Alikuwa akiwaza ni nini imefanyika kwa Danieli. Hakuweza kukula wala hakutaka kusikiliza muziki. Aliamka asubuhi na mapema na kwenda kwenye tundu la simba. Mungu alikuwa ameokoa Danieli au simba wamemkula?



**33.5** Mfalme Dario aliita Danieli, "Danieli, Mungu wako ameweza kukuokoa kutoka kwa simba?" Akasikiliza na akajibiwa, "Mungu alituma malaika na wakafunga midomo ya simba hawajaniumiza." Mfalme alifurahi alipoona kwamba Danieli amepona. Aliamrisha kwamba Danieli atolewe kwenye tundu la simba. Danieli aliondolewa na hakukuwa ameumizwa hata kidogo. Mungu alimwokoa kutoka kwa simba kwa sababu aliamini Mungu na kumtii.

Lakini wale mawaziri waovu waliopanga kumuua Danieli, walitupwa kwa simba na wakauwa wote.